# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**MOI GIRLS HIGH SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# MOI GIRLS SCHOOL - NAIROBI KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/1**

**Karatasi ya 1**

**Mwongozo wa kusahihisha**

**Swali la 1.**

- Mwanafunzi azingatie muundo / sura ya ripoti Kichwa kionyeshe ripoti ya nani / kamati gani, kuhusu nini n.k

**Utangulizi.**

- Mtahiniwa aeleze
- Dhamira ya kamati
- Wanakamati pamoja na vyeo vyao.
- Muda ambao kamati ilichukua kufanya uchunguzi.
- Mbinu za ukusanyaji data.

**Mwili.**
Mtahiniwa zingatie;

(a) **Sababu za kuzorota kwa elimu - mfano**

- Kuzorota kwa nidhamu.
- Upungufu wa walimu.
- Kutamauka kwa wanafunzi kutokana na ukosefu wa kazi.
- Shinikizo la marika.
- Umaskini - wengi wanajihusisha na ajira.
- Wazazi kutowajibika katika malezi.
- Matumizi ya dawa za kulevya. n.k

(b) **Matatizo waliyopata.**

- Uchechefu wa fedha
- Ukosefu wa hamasa miongoni mwa waliohojiwa.
- Ukosefu wa mahali pa kukutana. n.k

(c)**<u>Mapendekezo</u>.**

- Yaambatane na hoja za mwanafunzi.

(d)**<u>Hitimisho.</u>**

- Atoe maoni yake kwa kifupi kuhusiana na suala hili.

**<u>Swali la 2</u>.**
Athari nzuri / chanya.

- Kuchangia katika elimu - intaneti.
- Kupasha habari kuhusu mambo mbalimbali.
- Husaidia kuboresha uwezo wa mawasiliano na lugha.
- Ni msingi wa burudani katika maisha yetu.
- Hurahisisha kazi na kuokoa wakati.
- Hufanya kazi nyingi.

**<u>Athari mbaya / hasi.</u>**

- Kuweza kutekwa na tarakilishi kiasi cha kuwa na uraibu usioepukika.
- Kuingizwa kwenye utamaduni mwingine kwa kutazama visa na mambo mengine ya kigeni.
- Kuna mambo yanayoweza kuwa ya fedheha na hasa ikiwa watu wanaotumia tarakilishi waheshimiane.

- Huathiri fikra hasa kutokana na ponografia.
- Kupunguza nafasi za kazi.
- Kuwafanya watu kuwa wavivu.
- Baadhi ya mataifa huwa majaa ya kutupa tarakilishi zilizoharibika - uharibifu wa mazingira.

**Tanbihi**.

- Mtahini ahakiki hoja zaidi za watahiniwa.
- Mtahiniwa azingatie tarakirishi si uvumbuzi mwingine.
- Mtahiniwa aonyeshe sehemu zote mbili japo si lazima idadi ya hoja iwe sawa.
- Akizingatia upande /sehemu moja asipite kiwango cha C+

- **Swali la 3**
- Fahali wawili - Watu wawili wenye nguvu wanapopigana hawaumizani bali nyasi / watu wa kawaida ndio
- huumia.
- Mtahiniwa atunge kisa kudhihirisha hali hii.
- Akitunga kisa kisichooana na methali hii amejitungia swali na kujibu. Awekwe katika kiwango
- cha D- (01/02)
- Pande zote mbili za methali zionekane.

**Swali la 4**

- Mtahiniwa aweze kujenga kisa ambacho kinamhusisha yeye mwenyewe kama mhusika mkuu.
- Akimjenga mhusika mkuu mwingine amepotoka (D 03)

- Mtahiniwa asibadili wakati uliohusika katika swali.  Akifanya hivyo amepotoka.

**TANBIHI**.

- Mtahini azingatie viwango vya utuzaji katika kutuza.

- Viwango vyenyewe ni A, B, C, D